**Propaganda za mahusiano humaanisha nini ?**

Propaganda za mahusiano ni mchanganyiko wa habari,maneno na matendo yanayopangwa kwa makusudi ili kuathiri namna watu watu wanavyoona au kuamini kuhusu mahusiano yao.

Mara nyingi huwa na lengo la kuchochea hisia fulani ili kuvuruga au kudhoofisha uhusiano.

Huu ni mchakato wa kueneza taarifa, hisia au mitazamo iliyo andaliwa kwa makusudi ili kuongoza wahusika waanze kuamini, kufikiri au kujihisi kwa namna fulani ambayo muhusika ametaka, kwa lengo la kudhibiti maamuzi yao juu ya uhusiano.

Pia inaweza kuwa ni njia ya kupindisha au kukata taarifa kwa makusudi, ili kuathiri hisia na maamuzi ya mwenza kwa ajili ya kudhibiti mtazamo wake juu ya uhusiano.

Propaganda ni nguvu ya kuwaongoza watu wengine kwenye uelekeo unaoutaka kwa kutumia mawazo na mtazamo wako unaotaka.

Hata hivyo jamii yetu imekuwa muathilika zaidi wa propaganda, kwa sababu tumekuwa watu wa kuiga namna fulani ya maisha, mitazamo na hata maarifa ya namna ya kuendesha mambo fulani kwenye maisha.

Hii imeingia hadi kwenye mahusiano.

Mahusiano mengi yameangushwa na kuvunjika kupitia tu propaganda. Vitu unavyoaminishwa ni ukweli na kumbe si hivyo.

Lengo kuu la propaganda za mahusiano ni kushawishi upande mmoja au pande zote mbili kuamini taswila fulani kuhusu mahusiano yao ambayo kiuhalisia haipo hivyo.

Hii hali hupunguza uaminifu, huongeza mashaka na kuongeza migogoro inayoweza kuleta hatima ya kuvunjika kwa uhusiano.